
# Mwongozo wa Uinjilisti na Uanafunzi




## Maswali Manne ya Kufundisha

Soma **Mathayo 28:18-20**. Yesu anasema **mkawafanye kuwa wanafunzi**. Mafunzo haya yanajenga Wakristo ili wakaweze kuwafanya watu kuwa wanafunzi kwa kujibu maswali manne.

### 1 Kwa Nini?→**Utambulisho**

**2 Wakorintho 5:17-20**





**Soma 2 Wakorintho 5:17-20**

**Msalaba**: Tunaposoma katika vifungu hivi tunaona kwamba ukiwa ndani ya Yesu Kristo kuna vitu viwili za ukweli ndani yako kwa sababu ya Yesu. **Hauwezi zitenganisha.**

**Mstari 17 (Mtu)** Umefanywa kuwa kiumbe kipya. Umesamehewa dhambi zako zote.

**Mstari 20 (Ulimwengu)** Amekupa utambulisho mpya kama balozi wake.

### 2 Nani?→**Ramani ya Oikos/Boma**





* Matendo 16:30-33


Andika majina ya watu katika Maisha yako walio mbali na Mungu.

### 3 Nini?

**Sekunde 15 za Ushuhuda**





### 4 Lini? → **Kuweka Malengo**


- Maombi
- Kushiriki



Kila Saa ______________________

Jina / Muda ______________________

**Falme Mbili**



## Falme Mbili

Falme mbili ni mfano ambao Yesu alitumia kueneza Habari njema kwa wakati aliishi hapa ulimwenguni. Ni vyema kuelewa ujumbe wa Yesu na ni jukumu letu pia kuieneza Habari njema. Habari hii tunaipata katika **Wakolosai 1:13-14.**

**Chora duara mbili, ya kwanza iwe juu na ya pili iwe chini.** Kuna falme mbili katika ulimwengu huu. Ufalme wa Mungu ni nzuri, kamilifu na umejawa na upendo. Vile vile, ufalme wa pili ambao ni ufalme wa giza uliyojawa na uharibifu kwa sababu ya kutotii kwa mwanadamu.

Mpango wa Mungu tokea mwanzo ulikuwa kuwa mwanadamu aishi katika ufalme wa mwangaza. Katika hii ufalme, Yesu ndiye Bwana. Ni ufalme ulio na amani na uhuru kutoka kwa dhambi. Wanainchi wa ufalme huu, wanamfuata Yesu kama mfalme na wanaishi kulingana na njia zake.

**Fafanua ufalme wa giza.** Ufalme huu unatawaliwa na shetani. Katika huu ufalme, unashawishiwa kufuata njia za ulimwengu, shetani, na ubinafsi. Ni ufalme uliojawa na uchungu na kilio. Kwa sababu hiyo, watu hujaribu kuepuka kupitia pesa, mali, jamii, au dini. Lakini hizo zote haziwezi kututoa katika ufalme wa giza. Ni kama bendi ya elastiki (blada) ambayo huvutika. Inaweza kukufanya usikie vizuri kwa muda lakini mwishowe unarudi pale pale ulikotoka kwa uharibifu. Ufalme huu ni ufalme ulioharibika.

**sasa linganisha falme hizi mbili.** Katika ufalme wa mwangaza tunayo upendo, lakini katika ufalme wa giza kuna chuki na uharibifu. Katika ufalme wa mwangaza kunayo uhuru, lakini katika ufalme wa giza kunayo ufungwa. Katika ufalme wa mwangaza, kunayo amani tele ilhali katika ufalme wa giza kunayo hasira. Katika ufalme wa mwangaza, kunayo uzima, ilhali katika ufalme wa giza kunayo mauti.


**Kwasasa ifanye uwasilishaji wako uwe kibinafsi.** Muulize unayeshiriki naye, “unafikiria upo katika ufalme gani sasa?” “Ni ufalme gani ungependa kuwepo?” Haijalishi ni jibu gani alilokupa katika swali la kwanza. Kama jibu lao lilikuwa, “ndio ninataka kuwa katika ufalme wa Mwangaza,” basi shiriki nao habari njema.

**Chora msalaba katikati ya duara mbili ulizochora hapo awali.** Habari njema ni kwamba Mungu alikuwa na mpango wa ukombozi tokea mwanzoni. Alimtuma mwanawe Yesu Kristo kuturejesha katika ufalme wa mwangaza. Bibilia inasema katika **Yohana 3:16** “Kwa maana jinsi huu, Mungu aliupenda ullimwengu hata akamtoa mwana wake wa kipekee.” Yesu alikuja ulimwenguni na akaishi Maisha isiyo na dhambi **(Chora mstari kutoka duara la mungu hadi duara la shetani).** Aliishi Maisha ya utiifu bila kuasi na kutofuata uongo wa ufalame wa giza. Yesu aliishi Maisha kamilifu, pasipo kuasi nahata akafa msalabani ili mimi na wewe tusipitie kifo kama yake. Alizikwa, na akafufuka ili yoyote atakaye kiri Warumi 10:9 atakuwa na uzima wa milele. **(Chora mstari kutoka ufalme wa giza kuelekea ufalme wa mwangaza)**. Tunapomwamini Yesu, anatupa uzima wa milele. Tunasamehewa na kupewa fursa ya kuwa katika ufalme wa Mwangaza.

**Maliza hivi.** “Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, ya ukweli, na uzima. Hakuna aendae kwa Baba ila kupitia kwangu mimi” **(Yohana 14:6)**. Tukihitaji kuwa katika ufalme wa mwangaza, ni lazima iwe kupitia kwa Imani kwa Yesu Kristo. Tunapomwamini Yesu na kuweka Imani yetu kwake, basi Biblia inasema ya kwamba tutakombolewa kutoka kwa giza na kupelekwa katika ufalme wa Mwangaza **(Wakolosai 1:13)**. Waulize, “Je ungependa kumpokea Yesu leo hii, ili utoke katika ufalme wa giza hadi katika ufalme wa mwangaza?”

**Wape muda wa kujibu.** Kama wako tayari, wasadie katika maombi ya kutubu na Imani ili wakazaliwe kwa mara ya pili. Kama hawako tayari, basi omba Pamoja nao na utafute wakati mwingine wa kuongea Zaidi kuhusu Habari njema.

**Duara Tatu**



Uumbaji Kamili wa Mungu
Upotevu
1. Tubu & 2. Uamini
Yesu
Kukuwa kwa Kristo & Enenda

## Duara Tatu

Duara Tatu ni mbinu maarufu ya kushiriki habari njema, kama vile Falme Mbili. Inaonyesha jinsi ambavyo Mungu aliiumba ulimwengu, jinsi ambavyo ardhi iliingiwa ufisadi, na jinsi ambavyo Yesu anatupatanisha naye Mungu.


**Chora duara mbili; moja karibu na nyingine.** Ulimwengu wetu uliovunjika umejawa na ugomvi na dhambi. **Chora zigizagi ndani ya duara lile la pili kuonyesha kuwa limevunjika**. Wakati mwingine watu hutumia pesa, pombe, madawa ya kulevya na vitu vingine ili kuepuka shida zao, lakini kama elastiki (blada), wao bado hurudi pale pale katika ulimwengu uliovunjika. **Chora mishale zikitoka kwenye dunia iliyo vunjika kuonyesha vile watu wanajaribu kutoka kwenye dunia yenye maumivu na mateso**. Watu hutumia vitu hivi kujaribu Kurekebisha maisha yao, lakini kila mara wao hurudi pale katika ulimwengu uliovunjika. Kuvunjika kwetu hakukuwa mpango wa Mungu. Mungu aliuumba ulimwengu uliokamilika, lakini watu walidhihaki na kupoteza uhusiano wao na Mungu. **Chora mshale kutoka kwenye dunia iliyo kamili hadi kwenye dunia iliyo vunjika kuonyesha vile mwanadamu alitolewa kutoka kwa mpango wa Mungu kupitia dhambi.** Je wakubali kuwa ulimwengu huu umevunjika/kuharibika?

**Chora/eleza duara kamilifu la Mpango wa Mungu.** Mpango wa Mungu tokea hapo mwanzo, ulikuwa ulimwengu kamilifu ulio na upendo bila dhambi. Mungu aliuumba ulimwengu uliyo kamili na tamaa yake ilikuwa uhusiano kamili na mwanadamu. Hata hivyo, kupitia dhambi au kutotii kwa Adamu na Awa uhusiano huu kamili ulivunjika. Matokeo yake ni kuwa uhusiano wetu na Mungu haiwezi kuwa kama ilivyokuwa hapo awali na tumebaki kuvunjika. **Muulize mtu unaye muongelesha akuoneshe duara gani inayowakilisha maisha yake.** Ikiwa atakuonesha kuwa anaishi katika ulimwengu ulio kamilika, muulize jinsi ambavyo alifika hapo. Ikiwa atasema ni muumini lakini hawaelewi habari njema vyema, au hawezi kuieleza, endelea katika duara la tatu. Ikiwa atasema kuwa maisha yake inakaa kama ulimwengu uliovunjika, muulize, je ni ulimwengu gani angependa kuwepo? Ikiwa atasema angependa kuwa katika ulimwengu uliyo kamilifu, muelekeze katika duara la tatu.

**Chora duara ya tatu chini ya zile mbili za kwanza**. Kuna njia moja tu ambayo tunaweza kutoka katika hali ya kuvunjika hadi katika uhusiano kamili na Mungu, na ni kupitia kwa kuwa na uhusiano na Yesu Kristo. Yesu ndiye mwana wa Mungu, na ni yule aliye kuja hapa duniani (**mkuki unaotoka juu mpaka chini**) akafa msalabani, na akafufuka siku ya tatu (**mkuki unaotoka chini kwenye dunia iliyo vunjika hadi kwenye dunia iliyo kamili**). Kwa kufufuka kwake, alidhihirisha kuwa yeye ni Mungu na ameshinda mauti, akalipa deni ya dhambi zetu. Yesu ndiye njia pekee ya kuturejesha katika mpango kamilifu ya Mungu, tukitubu na kumwamini **(Andika Kutubu & Kuamini). Sasa chora laini kutoka dunia iliyo vunjika hadi kwa Yesu, na kutoka kwa Yesu hadi kwenye mpango kamili wa Mungu.** Ikiwa mtu atatubu na kuweka imani yake kwa Yesu basi ataokolewa. Wakati Yesu ametuokoa, Yeye hutubadilisha halafu tunaanza kukua kiroho. Katika **Yohana 14:6**, Yesu anasema, “Mimi ndimi njia, na ukweli na uzima. Hakuna awezaye kwenda kwa Baba ila kwa kupitia kwangu.” Inawezekana kutoka katika ulimwengu huu uliovunjika, iliyo na dhambi na uchungu kwenda katika mpango wa Mungu ambapo tutashiriki katika uhusiano wa kudumu. **Uliza mtu au watu waliyosema hawapo kwenye dunia ya mungu kama wangependa kutubu na kumuamini Yesu**. Wape nafasi ya kuomba ombi la kutubu kwa imani ndio wapate kuepuka ulimwengu uliovunjika, kwa njia ya kumwamini Yesu.

**Maono ya kutumwa - kwa wokovu wapya.** Kitu kizuri, ni kuwa Mungu anataka tupeleka habari hii kwa ulimwengu wote. Yesu alikuja duniani, akafa, na akafufuka kuwaokoa wale waliotubu na Kumwamini. Yesu anataka tumfuate na tuwe wavuvi wa watu kwa ajili yake (**Marko 1:17**). Bado tunayo kazi katika ulimwengu huu uliovunjika. Yesu anatutuma turudi katika ulimwengu uliovunjika kushiriki habari ya wokovu kwa waliopotea ili wakazaliwe kwa mara ya pili (**Chora laini na uandike “kua na nenda.”)** Ingawa bado tuko katika ulimwengu uliovunjika, tunaweza ishi katika mpango wa Mungu aliyoipangia maisha yetu. Hatupaswi kuwawacha wengine katika ulimwengu uliovunjika, ilhali tunafaa kuwasaidia kumpata Yesu kwa kushiriki habari njema nao.

**Hesabu na Usherekee**



| X | ? | ✓ | ✝ |
|---|---|---|---|
| Hana nia<br><br>Ondoka | Kuna uwazi wa kujifunza<br><br>Rudi tena | Amekuwa muumini<br><br>Mkaribishe kanisani/uanafunzi | Tayari yu muumini<br><br>Mfunze kueneza injili |

| Matokeo ya Kueneza Injili | |
|---|---|
| **Alama** | **Nambari** |
| **X** | |
| **?** | |
| ✓ | |
| ✝ | |
| **Total** | |

**Mafundisho ya Muda Mfupi**

Mafunzo haya yameundwa ili kuwasaidia waumini kuelewa vipengele muhimu katika kanisa. Kila kifungu kimechagulia kwa uangalifu ili kusaidia kikundi kugundua maana ya kumtii Kristo. Tumia Mbinu ya kujifunza somo la Biblia ili kugundua Maandiko yanasemaje.

Kukariri Biblia ni jambo la muhimu ili kuweza kupigana dhidi ya dhambi, kuwaongoza watu katika Kristo, na kukua kama mfuasi wa Mungu. **Zaburi 119:11 yasema, "Nimelificha neno lako moyoni mwangu ili nisikutende dhambi."** Kariri kifungu hiki kifuatacho cha Biblia na kila somo lililosomwa.

| Kumbukumbu ya Maandiko | Hadithi | Maandiko ya ziada | Andiko la kukariri | Kamilisha ✓ |
|---|---|---|---|---|
| 1. Kuamini na Kutubu | 1. Luka 7:36-50 | Warumi 3:23, 6:23, 10:9-10 | 1. Mathayo 4:17 | |
| 2. Ubatizo | 2. Matendo 8:26-39 | Mathayo 3:13-16; Warumi 6:3-4; Matendo 2:38 | 2. Mathayo 28:19 | |
| 3. Maombi | 3. Mathayo 6:5-15 | Luka 10:2 | 3. Mathayo 6:9-13 | |
| 4. Kuwafanya wanafunzi | 4. Yohana 4:4-42 | Luka 10:1-11 | 4. Mathayo 28:19-20 | |
| 5. Upendo | 5. Luka 10:25-37 | Yohana 13:34-35, 14:15, 15:13, 21:17; 1 Wakorintho 13 | 5. Mathayo 22:37-39 | |
| 6. Kuabudu | 6. Matendo 16:25-34 | Zaburi 100 | 6. Mathayo 4:10 | |
| 7. Meza ya Bwana | 7. Luka 22:7-20 | 1 Wakorintho 11:23-29, Matendo 2:42 | 7. Luka 22:19-20 | |
| 8. Sadaka/Kutoa | 8. Marko 12:41-44 | Mathayo 6:1-4, Matendo 4:34-35; 2 Wakorintho 9:6-7 | 8. Mathayo 6:1-4 | |
| 9. Kusanyiko | 9. Matendo 2:36-47 | Matendo 5:42, 17:5-7, 18:7, 19:9, 20:20; Warumi 16:1-5; 1 Wakorintho 10:31, 16:19; Wakolosai 4:15; Filemoni 1:1-2 | 9. Waebrania 10:24-25 | |

**Mafundisho ya muda mrefu**

Tumia muundo sawa na uliyoitumia katika mafundisho ya muda mfupi kuisoma Injili ya Marko. Kitabu cha Marko inasaidia kusanyiko kuelewa kitabu chote cha Bibilia, na sio hadithi moja tu. Injili ya Marko ni fupi kati ya Injili zote nne na inaangazia maisha ya Yesu. Kila funzo ni chini ya mistari 25 ya kila mlango katika kitabu cha Marko. Kwa hivyo yawezekana kumaliza mafunzo haya kabla ya mwaka kuisha. Pale unapomaliza fikiria kusoma Matendo au Yohana.

| **Marko Kusoma** |
|---|
| 1. 1:1–20 (20) |
| 2. 1:21–39 (19) |
| 3. 1:40-2:12 (18) |
| 4. 2:13–28 (16) |
| 5. 3:1–12 (12) |
| 6. 3:13-35 (23) |
| 7. 4:1-20 (20) |
| 8. 4:21-41 (21) |
| 9. 5:1-20 (20) |
| 10. 5:21-43 (23) |
| 11. 6:1-13 (13) |
| 12. 6:14-30 (17) |
| 13. 6:31-44 (14) |
| 14. 6:45-56 (11) |
| 15. 7:1-13 (13) |
| 16. 7:14-23 (10) |
| 17. 7:24-37 (14) |
| 18. 8:1-10 (10) |
| 19. 8:11-30 (20) |
| 20. 8:31–9:13 (21) |
| 21. 9:14-29 (16) |
| 22. 9:30-50 (21) |
| 23. 10:1-16 (16) |
| 24. 10:17-31 (15) |
| 25. 10:32–52 (21) |
| 26. 11:1-11 (11) |
| 27. 11:12-33 (22) |
| 28. 12:1–12 (12) |
| 29. 12:13-27 (15) |
| 30. 12:28–44 (17) |
| 31. 13:1-23 (23) |
| 32. 13:24-37 (14) |
| 33. 14:1-11 (11) |
| 34. 14:12-31 (20) |
| 35. 14:32–52 (21) |
| 36. 14:53–72 (20) |
| 37. 15:1-20 (20) |
| 38. 15:21-32 (12) |
| 39. 15:33-47 (15) |
| 40. 16:1-20 (20) |

## Mbinu ya Kujifunza Somo la Biblia

Mafunzo ya Biblia ni Njia ya Kuwafunza Wakristo Kuelewa neno la Mungu wao wenyewe.

**Maana ya Biblia hutoka katika aya, sio katika sentensi au neno.** Unapojifunza Biblia, soma aya na simuliza yote. **Kwa kila nakala, na maswali yawe na majibu mengi.**

1. Tunajifunza nini kumhusu Mungu?
2. Tunajifunza nini kuhusu watu?

Unaposoma maandiko, baadhi ya maswali haya huenda hazitakuwepo au kuwepo. Uliza kila swali uone kilicho ndani ya ujumbe.

A. Je kuna dhambi ya kuepuka?
B. Je kuna ahadi ya kudai?
C. Je kuna mfano wa kufuata?
D. Je kuna amri ya kutii? [1]

[1] Kevin Rodgers, "Healthy Church Leadership: A Manual for Healthy Churches in Africa" (IMB, 2021), 3–4.

## Mikutano ya Msalaba

Tutatumia mfumo wa mikutano ya msalaba ili kuweka uwajibikaji na Ni namna gani watu walivyoshiriki kwa uaminifu kazi ya juma lilopita.

### Tazama Nyuma

**1. Uchungaji:** Mjigawe katika vikundi vidogo vya watu wawili au wanne kwa kusudi la kuulizana maswali ili kuona vile ambavyo watu wanaendelea kimwili, kiroho na kihisia katika maisha yao ya kila siku.

**2. Uwajibikaji:** Kila mtu aeleze vile alikua mwaminifu kufuata na kuvua kwa ajili ya Kristo.

**3. Maombi:** Omba na umualike roho mtakatifu.

**4. Abudu:** Imba wimbo moja au mbili kwa Mungu kwa mujibu wa wema wake.

**5. Utoaji wa Maono**: Shiriki hadithi au mawazo yanayo changia katika maono yanayo sisimua watu kuhusu mafundisho na masomo.

### Tazama Juu

**6. Somo Mpya:** Pengine huko kuna ujuzi wa kujifunza kama vile uinjilisti na vifaa ya kujifunzia Biblia. Hakikisha unafanya mazoezi na wengine.

**7. Mazoezi ya Soma:** Hakikisha lazima kila mmoja anaelewa lengo kila wiki.

### Tazama Mbele

**8. Lengo la Kuwafuata na Kuwavua:** Kila mmoja ni lazima kupanga lengo la kila wiki. Uvuvi kwa Yesu ni kushiriki habari za Yesu kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa watu waliombali na Mungu. Kupitia somo kila wiki. Kuwa mfuasi wa Mungu ni kusoma Biblia angalau sura moja kwa siku na kumfuata Mungu kulingana na somo ulilolisoma katika Bibilia. Wakati mwingine hii huhushisha kujitolea kubatizwa, kuwasadia wasiojiweza, au kufanya upatanisho na wengine. Shiriki matokeo ya jukumu hili wiki ijayo wakati wa uwajibikaji.

**9. Maombi:** Omba washiriki watimize ahadi zao kwa Mungu na kubaki waaminifu kueneza injili.

**10. Kutuma Nje:** Maombi kwa ajili ya kuwatuma washiriki ili kuwafanya wengine kuwa wanafunzi.[2]

---

[2] Ibid., 3–4.


**Mafunzo Zaidi ya Uanafunzi**

Masomo haya yatatumika wakati maswali yameibuka kuhusiana na kanisa. Yanaweza kutumika kurekebisha makosa kanisani na kusaidia mwili wa Kristo kuwa katika afya bora kwa kusoma na kuelewa maandiko.

| |
|---|
| 1. **Uwajibikaji na Nidhamu:** Mathayo 18:15-20 |
| 2. **Uinjilisti:** Luka 10:1-23 |
| 3. **Uongozi:** 1 Timotheo 3:1-13 |
| 4. **Ushirika:** 1 Wakorintho 12:12-31 |
| 5. **Umisheni/Utume:** Warumi 10:13-17 |
| 6. **Kuhubiri na/Kufundisha:** 2 Timotheo 4:1-8 |
| 7. **Uhakika wa Wokovu:** Yohana 10:1-18; 1 Yohana 5:11-12 |

## Moyo ya Baba Wetu

Habakuki 2:14





Haja ya moyo wa Baba wetu ni utukufu wake. **Habakuki 2:14 Kwa maana dunia itajawa maarifa ya utukufu wa bwana kama maji yaifunikavyo bahari.** Sababu kuu ya kufanya umishonari ni kuumpa Mungu utukufu na Heshimu. Maono kuu ya mbinguni ni kuona kila kabila, lugha na mataifa yakizingira kiti cha enzi chake Mungu wakimwabudu na kumheshimu (**Ufunuo 7:9**). Kuwafikia waliopotea katika Kristo, kupanda makanisa, na kupanua ufalme wa Mungu sehemu zote za ulimwengu zaleta utukufu kwa Mungu. Kwa hivyo kipengele cha kwanza cha kukumbuka ni kuwa **haja ya moyo wa baba wetu ni utukufu wake (imeashiriwa na mistari ambazo zatoka kutoka kwa moyo).**

**Jinsi ambavyo Baba wetu hueneza utukufu wake katika sehemu zote za ulimwengu ni kupitia kuwaleta watu kwake.** Kwa sababu anaipenda ulimwengu(Yohana 3:16), tamaa yake ni kuokoa waliopotea na kwa hivyo ameipatia kanisa jukumu kuu (Mathayo 28:18-20) la kulileta ulimwengu uliopotea kwa Kristo. **Mungu hueneza utukufu wake katika sehemu zote za ulimwengu kupitia kanisa la mtaa** (imeashiriwa na jingo la kanisa). **Mungu hutumia watu binafsi,** lakini hao watu binafsi lazima wawe na uhusiano, na wawe sehemu katika kanisa la mtaa. Lazima wawe watu wa **maombi** (imeashiriwa na mtu aliyepiga magoti), ni watu ambao **wanakaa ndani ya Kristo** (imeashiriwa na mtu aliye na moyo mkubwa), na ni watu ambao huenda kwa **majirani zao na Habari njema ya Kristo** (imeashiriwa na mshale kwenye mlango).

Kanisa ndicho chombo ambacho Mungu hukitumia kueneza utukufu wake katika sehemu zote duniani. Makanisa haya yapo na waumini wa kweli ambao wana kaa katika Kristo, maombi, kuabudu na kushiriki Habari njema na waliopotea. Makanisa wanapotimiza jukumu kuu la kueneza Habari njema kwa ulimwengu( imeashiriwa na mshale uliopinda) basi utukufu wa Mungu unadhihirika katika dunia. Huu ndio mpango na kusudi kuu la Mungu.

**Uwanja/Shamba: Mfumo wa Kazi ya Mmishonari**




Hii ina tolewa kwa mafundisho ya Kristo katika Marko 4:26-29. Mungu hutumia watu kutoka makanisa ya mitaa kuingia mashamba mapya, kushiriki injili, kuwafunza wanaookoka, kuanzisha makanisa yenye afya, kufunza viongozi na kuondoka kuendelea na ushirikiano.

**1. Kuingia:** ukiingia uwanja mpya kuna kueneza injili kwa uwazi na upana, mfano; kuomba na kujenga uhusiano. Kwa uwanja huu, mpanzi (Mkristo) ana panda mbegu (injili). Yesu kwa Marko 1:17 alimwambia Petro, " **Nifwate nanitakufanya mvuvi wa watu,**" hii inamaanisha kwamba Mkristo lazima amfwate Yesu na amvulie. Mungu tayari anatayarisha mavuno (Luka 10:2). Kuna aina mbili ya watu; **Waliookoka na Waliopotea.** Tukikutana na aliye potea, tunafaa kushiriki injili. Na tukikutana na aliyeokoka yafaa kumfunza kumfuata Yesu na kukuwa mvuvi wa watu.

**2. Uinjilisti wa kibiblia:** Baada ya kuingia shamba, kupata walio potea na kushiriki injili. Wakiokoka wafunze kushiriki injili**. Tumia mbinu rahisi ya kueleweka na ambayo yaweza kurudiwa tena.**

**3. Mafunzo ya kibiblia ya wanafunzi:** Wahimize walio okoka kujiunga na kikundi kidogo cha kusoma Biblia (watu 5-10). Someni mafundisho mafupi (masomo 12) alafu mafundisho marefu (Miezi 6-8), **ukisisitiza kutii na uadilifu.**


**4. Kanisa lenye afya:** Hawa Wakristo wa hiki kikundi kidigo yafaa waanze kujiona kama Kanisa. Eleza maana yakukuwa kanisa na nini ni kanisa lenye afya (Matendo 2:36-47). Ukitumia **Mbinu ya Msalaba,** wafunze ukitumia Biblia kuwaeleza jinsi ya kukutana kama Kanisa. **Kanisa ni watu na sii jengo** (1 Wakorintho 12:12).

**5. Ukuzaji wa Uongozi na Elimu ya Kitheolojia:** Hii huanza na uinjilisti na kuwafunza wengine kushiriki imani yao. Jinsi makanisa yanavyoundwa, viongozi lazima wafundishwe. Viongozi wa makanisa mapya wanapaswa kushirikishwa katika somo la Biblia na kutumika kama Kristo (Wafilipi 2:5-8). **Viongozi lazima wawe waaminifu, wapatikane, na waweze kufundishwa.**


**6. Toka kwa Ushirikiano:** Huu ni mchakato endelevu. Hii inaitwa "Shamba" kwa sababu ni sehemu moja yenye shughuli tofauti zinafanyika kwa wakati mmoja. Makanisa hayawezi kuwa na afya isipokuwa yanapanda makanisa mapya. Ufalme wa Mungu huenea wakati makanisa yanapopanda makanisa zaidi. Mfano (kuwa mfano), Saidia (wasaidie kujifunza), Tazama (wape ushauri), Ondoka (nenda lakini endelea kushikamana).

## Mviringo wa Kanisa

1. Chora mviringo wa duara kuonesha mkusanyiko wa waumini.



2. Matendo 2:36-47 hizi ni kazi tisa za afya ya kanisa. Kutubu na kuamini, ni namna mtu anavyoweza kujiunga na kanisa.






Mshale huonyesha kutubu na kuamini.

3. Kama unafanya kazi yoyote ya sehemu hizi tisa katika kikundi chako. Liweke ndani ya duara. Kama hulifanyi weka nje ya duara.



4. Kama kikundi chako lakusanyika kama kanisa, tengeneza duara iliyo imara.



Kila wiki andika orodha ya:
**Watu waliohudhuria:**
**Waumini:**
**Waliobatizwa:** [3]

[3] Based on George Patterson's *7 Commands of Christ.*